

**MUHTASARI WAS KIKAO CHA DHARULA CHA BODI YA ZABUNI  
KILICHOFANYIKA KATIKA OFISI ZA MANUNUZI TAREHE 22/10/2021**

**WALIOOHUDHURIA**

S/N	JINA	CHEO	CHEO KWENYE BODI
1.	Cheyo P. Nkelege	Afisa ardhi (W)	Mwenyekiti
2.	Bi. Neema Mwinyipembe	Afisa manunuzi msaidizi (W)	Katibu
3.	Rwegerela Katabaro	Afisa M/J (W)	Mjumbe
4.	George kasibante	Mganga Mkuu (W)	Mjumbe
5.	Elihuruma Nyella	Afisa Utumishi (W)	Mjumbe
6.	Bw. Edward Kutandikila	Mwanasheria (W)	mwalikwa

**SEKRETARIETI**

1. Farida Chusi
2. Neema Mwinyipembe
3. Restitute Ndudumizi

**AGENDA**

1. Kufungua kikao
2. Kusoma na kuthibitisha agenda
3. Kutoa idhini yakutekeleza manunuzi katika miradi ya UVIKO 19 kwa njia ya FORCE ACCOUNT
4. Mengineyo kwa idhini ya mwenyekiti

**MUH/CTB/NA.23/2021-2022: KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti alifungua kikao saa 4:30 asubuhi baada yakuwaomba wajumbe kuchangia nakujadili agenda zilizopo kwa umakini na maslahi mapana ya Halmashauri na Taifa kwa ujumla.

**MUH/CTB/NA.25/2021-2022: KUTOA IDHINI YA KUTEKELEZA MIRADI YA UVIKO 19 KWA KUFANYA MANUNUZI KWA NJIA YA FORCE ACCOUNT**

Katika agenda hii, katibu aliwasilisha taarifa inayoonesha fedha Tsh. 4,330,000,000 zimeletwa na serikali katika Halmashauri ya Wilaya Kilosa, kati ya fedha hizo, Tsh. 2,940,000,000, zitatumika kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 137 katika shule za sekondari 38. Tsh. 780,000,000 zitatumika katika ujenzi wa vyumba 39 vya madarasa katika shule za msing shikizi. Tsh. 90,000,000 zitatumika katika ujenzi wa nyumba ya mtumishi katika Hospitali ya Wilaya. Tsh. 420,000,000 zitatumika katika ununuzi wa X-Ray mashine pamoja na Tsh. 100,000,000 zitatumika katika ujenzi wa ICU katika hospitali ya Wilaya. Wajumbe walijadili na kutoa idhini ya kutekeleza nakufanya manunuzi katika miradi hiyo kwa njia ya "FORCE ACCOUNT".

**MUH/CTB/NA.26/2021-2022: MENGINEYO**

Katika kikao hiki hakukuwa na mengineyo

**MUH/CTB/NA.27/2021-2022: KUFUNGA KIKAO**

**Mwenyekiti alifunga kikao saa 6:00 mchana baada ya kuwashukuru wajumbe kwa michango na uvumilivu wakati wote wa kikao.**

**UMETHIBITISHWA NA**



.....  
**KATIBU**

30/11/2021

.....  
**TAREHE**



.....  
**MWENYEKITI**